# TARGETER WINGS
# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT
# GREDI YA NANE - 2026
# KISWAHILI: LUGHA

Wings 001

Muda: Saa 1 dakika 40

| | |
|---|---|
| Jina la Mwanafunzi ________________ | Nambari ya Mwanafunzi __________ |
| Jina ya Shule yako ________________ | Nambari ya Shule ______________ |
| Sahihi ya Mwanafunzi ______________ | Tarehe ______________________ |

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| Swali | Upeo wa alama | Alama ya mwanafunzi | Kiwango cha utendaji |
| 1-50 | Alama 50 | | |
| Jumla | 50 | | |

**KISWAHILI LUGHA**
**Karatasi ya 1**

**MAAGIZO KWA MWANAFUNZI**

1. Umepewa **kijitabu** hiki na **karatasi ya majibu**. Kijitabu hiki kina maswali **50**.
2. Jibu maswali **yote** kwenye **karatasi ya majibu** uliyopewa kujibia maswali na wala **sio** katika kijitabu hiki.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida, aina ya HB.
4. Hakikisha kuwa karatasi ya majibu uliyopewa ina:
   NAMBARI YAKO YA MTIHANI
   JINA LAKO
   JINA LA SHULE YAKO
   JINA LA SOMO
5. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
6. Kwa kila swali, **1 – 50** umepewa majibu manne, **A, B, C, D.** Chagua **jibu sahihi.**
7. Kwenye karatasi ya majibu, onyesha jibu sahihi kwa **kuchora kistari** katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa jibu sahihi.

**Mfano:**
**Katika kijitabu cha maswali: Chagua jibu mwafaka.**

25. **Kamilisha tashbihi hii:**
Alikuwa jasiri kama ____________
A. kivinimbi  B. nyuki
C. fisi  D. simba

**Jibu sahihi ni 'D'.**
**Katika karatasi ya majibu,** palipo na visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **25**, chora kistari ndani ya kisanduku chenye herufi **D.**

25. [A] [B] [C] [D]

8. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
9. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu, kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**
**Hakikisha kuwa kurasa zote zipo na maswali yapo ipasavyo.**

## SEHEMU A

## I. UFAHAMU WA KUSOMA

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 6:</u>***

Maradhi ni baadhi ya adui kwa maisha ya mwanadamu,wanyama na mimea. **<u>Maisha yangalikuwa aula sana humu</u>** duniani tusingalikuwa na magonjwa. Maradhi huletwa na viini mbalimbali ambavyo huathiri viungo vya mwili wa binadamu, wanyama na hata mimea.

Baadhi ya maradhi yanayomwathiri mwanadamu ni ya kuambukizwa kama vile **<u>kipindupindu</u>**. Ugonjwa huu hutokana na kutupa takataka ovyoovyo kwenye maji yanayotumiwa na mwanadamu, viini vyake huenezwa na nzi ambaye hupenda kula chakula kizuri na hata kichafu. Vitendo vya kuenda haja kubwa vichakani na matumizi yasiyofaa ya vyoo huzidisha kuenea kwa maradhi haya.

Maradhi mengine kama vile Malaria, huambukizwa na mbu. Mbinu bora ya kuzuia maradhi yanayoambukizwa na wadudu wengine ni kuangamiza wadudu hao kwa kupulizia dawa sehemu ambazo binadamu anaishi. Yapo pia maradhi yanayoletwa na ukosefu wa chakula bora: Mfano ni utapiamlo ambao huwashika watoto wanaokosa vyakula vya kujenga mwili. Aidha kunayo maradhi ya zinaa kama vile kaswende, kisonono na ukimwi. Magonjwa haya huambukizwa hasa kwa kujihusisha na ngono bila kinga.

Kuna pia magonjwa yasiyoambukizwa. Baadhi ya magonjwa haya hutegemea mazingira. Vyanzo vinaweza kuwa vyakula, vinywaji au vitu vya starehe kama vile sigara. Saratani ni moja kati ya magonjwa haya.

Jambo muhimu kwa binadamu ni kuzuia maradhi, kuzingatia usafi, kuishi katika mazingira safi na kuwa makini na mienendo ya maisha ni mbinu yakini za kujiepusha na maradhi. Usafi wa mazingira, nguo, mwili na hata tabia ni hakikisho thabiti la kuepuka maradhi.

---

1. Kulingana na aya ya kwanza:
   A. Maradhi ndio adui pekee kwa maisha.
   B. Maradhi huathiri chochote kilicho na uhai
   C. Maradhi husababishwa na wadudu ambao pia huyasambaza
   D. Maisha hayapendezi humu duniani.

2. Kauli, **"Maisha yangalikuwa aula sana humu duniani tusingalikuwa na magonjwa."** Ina maana kuwa:
   A. Maisha ni mazuri humu duniani.
   B. Magonjwa huyafanya maisha kuwa bora.
   C. Magonjwa huathiri ubora wa maisha.
   D. Maisha hayajawahi na hayatawahi kuwa mazuri duniani.

3. Chagua mbinu iliyo bora zaidi ya kuukabili ugonjwa wa Malaria.
   A. Kulala ndani ya chandarua kilichotiwa dawa.
   B. Kumeza vidonge kabla ya kuumwa na mbu.
   C. Kupulizia makazi yetu dawa ya kuwaua mbu.
   D. Kuangamiza sehemu mbu wanazaana.

4. Ni ugonjwa gani unaosababishwa na mwenendo mbaya?
   A. Ukimwi
   B. Utapiamlo
   C. Kipindupindu
   D. Malaria.



CamScanner

5. Kifungu hiki kimesisitiza jambo gani ili kujiepusha na maradhi?
A. Lishe bora na kudumisha usafi.
B. Kuyazuia magonjwa
C. Kufanya mazoezi na kudumisha usafi
D. Kupata matibabu ya haraka.

6. Methali, **"Mgonjwa haulizwi sanda"** ni moja kati ya methali zinazotaja mambo yanayohusiana na magonjwa na tiba. Chagua methali isiyohusiana na magonjwa na tiba.
A. Mwenye Kovu, sidhani kapoa
B. Mganga hajigangi
C. Kinga ni bora kuliko tiba
D. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo

## UFAHAMU

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 7 hadi 12:***

Nyani aliamua kuanzisha biashara ya kuuza vifaa vya elektroniki mtandaoni. Ingawa hakuwa na mtaji, marafiki zake walikuja pamoja na kila mmoja akampa kidogo alichokuwa nacho. Mzee Kobe naye alimpa mkopo na wakafanya makubaliano ya kurejesha mkopo huo kwa kiwango cha riba cha asilimia kumi na nne kwa mwaka. Bila kupoteza wakati, Nyani alifungua akaunti kwenye mitandao ya kijamii na kuanza kutangaza bidhaa zake. Baada ya muda, wateja waliongezeka na biashara yake ikanoga kwelikweli. Nia yake ya kuwa mjasiri amali akaiona ikitimia. Hata hivyo, mambo yalianza kuchukua mkondo mpya baada ya kupokea ujumbe kutoka kwa mteja wake mpya aliyeitwa 'Sungura'. Sungura alidai kuwa alikuwa nje ya nchi na alihitaji tarakilishi. Baada ya makubaliano kuhusu malipo, alimwambia Nyani kwamba angemtumia malipo ya tarakilishi kwenye akaunti ya benki mara moja. Ingawa Nyani aliuza tarakilishi kwa **bei rafi** aliamua kumuuzia kwa bei aliyoipunguza akilenga wateja zaidi kutoka nchi za nje. Sungura alimwambia kuwa tayari alikuwa ameanzisha mchakato wa kumtumia hela zake.

Nyani akawa na furaha kuwa biashara yake ingenawiri zaidi akipata angalau wateja kumi kama Sungura kutoka nchi za nje. Alimtumia mteja lakini ngoja ngoja hiyo ikachukua siku nyingi. Alipojaribu kuwasiliana naye kwa njia ya simu na kwenye mitandao ya kijamii hakuweza kumpata. Hapo ndipo alipogundua kuwa amelaghaiwa. Akajuta na akajifunza kuchukua tahadhari na kufahamu kuwa malipo hufanyika kwanza kabla ya kuwatumia wateja asiowafahamu bidhaa.

7. Kwa nini Nyani alianzisha biashara mtandaoni?
A. Alitaka kupata njia ya kujipatia riziki.
B. Bidhaa za kielektroniki huuzwa mtandaoni.
C. Alikuwa na pesa za kuanzisha biashara.
D. Lengo lake lilikuwa ni kuwa mjasiriamali maishani.

8. Je, unadhani ni kwa nini Nyani alituma mzigo kabla ya malipo kuthibitishwa?
A. Alitaka kutimiza mahitaji ya mteja wake.
B. Alitaka biashara yake inawiri.
C. Alishawishika na ujanja wa Sungura.
D. Alitaka apate wateja zaidi kutoka nchi za nje.



CamScanner

9. Nyani angefanya nini ili kuepuka hasara aliyopata ?

A. Kungoja apokee malipo kwanza kabla ya kutuma bidhaa.

B. Kumshtaki Sungura mahakamani kwa kosa la udanganyifu.

C. Kununua bima ya biashara baada ya kulipia bidhaa

D. Kufunga akaunti yake ya benki na kutoa hela zote.

10. Nahau, **'bei rafi'** imetumiwa kwenye kifungu. Maana yake ni;

A. bei ya juu

B. bei isiyopunguzwa

C. bei ya kudanganyana

D. bei kiasi; nafuu

11. Je, unadhani awali Nyani alikabiliwa na changamoto gani kabla ya kuanzisha biashara yake?

A. Ulaghai mtandaoni

B. Kuanzisha biashara mitandaoni

C. Ukosefu wa mtaji

D. Ukosefu wa ujuzi wa biashara.

12. Neno, **'tahadhari'** limetumiwa katika kifungu hiki. Lina maana gani?

A. Ujasiri

B. Ushauri

C. Uchunguzi

D. Umakini

**UFAHAMU**

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 13 hadi 17:</u>***

Tunapaswa kuwa makini na bidhaa au vifaa vinavyonunuliwa sokoni na madukani. Kuna bidhaa ambazo zina uwezo wa kuvunjika, kuvurugika, kubondeka au hata kuharibika kutokana na sababu mbali mbali. Kwa hivyo uangalifu na umakinifu huhitajika.

Mnunuzi anapaswa kuzingatia matumizi yanayofaa ya bidhaa au vifaa. Mfano unaponunua mashine kutoka dukani, zingatia vyema **<u>maelekezo</u>** yanayotolewa kuhusu namna ya kutumia kifaa hicho. Iwapo utakosea kufuata maagizo, kuna uwezekano wa mtambo kuharibika ama ukakosa kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

Sharti uhakikishe kuwa bidhaa zinazonunuliwa kutoka madukani ama sokoni ni salama kwa afya yako. Matumizi mabaya ya vyakula na vinywaji ni hatari kwa afya ya mnunuzi. Kila mnunuzi ahakikishe kuwa anatumia tu anachohitaji. Tufahamu kuwa bidhaa tunayonunua ina tarehe ya mwisho ya matumizi. Iwapo tarehe imepita au inakaribia kutimia, basi ni hatari tukiitumia. Bidhaa hiyo pia ina tarehe ambayo ilitengenezwa na pia kampuni iliyoitengeneza. Wewe mnunuzi ikague bidhaa vyema kabla kununua. Bidhaa zitumiwe kabla ya tarehe ya mwisho kufika. Bidhaa ambayo tarehe ya matumizi imepita ni hatari na inaweza kudhuru afya ya mnunuzi.

13. Kulingana na kifungu,

A. hatupaswi kununua bidhaa kutoka sokoni

B. Mara nyingi bidhaa zinazouzwa masokoni au madukani hazitimizi ubora unaohitajika

C. Maelekezo ya jinsi ya kutumia bidhaa ni muhimu.

D. Sio bidhaa zote zinazonunuliwa kutoka sokoni au madukani.



CamScanner

14. Kukagua bidhaa kabla ya kuinunua ni njia moja ya kukuza

A. uwajibikaji

B. uzalendo

C. umakini

D. matumizi yafaayo.

15. Athari ya kutofuata maelekezo kuhusu matumizi ya kifaa fulani ulichonunua ni:

A. Kifaa kufanya kazi kwa muda mfupi.

B. Kifaa kufanya kazi kwa muda mrefu.

C. Kifaa kutoharibika kazi ifaavyo.

D. Kifaa Kutotekeleza kazi ifaavyo

16. Kutumia bidhaa baada ya tarehe ya mwisho ya matumizi yake kupita husababisha:

A. Bidhaa kuharibika

B. Madhara kwa mtumizi.

C. Hasara kwa muuzaji

D. Matumizi mabaya ya pesa.

17. Chagua kichwa kifaacho kwa kifungu hiki.

A. Majukumu ya mnunuzi.

B. Matumizi yafaayo ya dawa.

C. Jinsi ya kutumia bidhaa zilizonunuliwa

D. Tarehe muhimu kwa matumizi ya bidhaa

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 18 hadi la 20**

Tiro, Kanyau, Godi na Andanje ni wateja wakuu wa Mzee Tamaa ambaye huwauzia Luzia bidhaa kwa bei rejareja na kisha hao wateja wake huuza bidhaa hizo kwingine. Kila mmoja huwa na siku ambayo hununua anachohitaji. Tazama jedwali hili.

| Siku / Bidhaa | Jumanne | Jumatano | Alhamisi | Ijumaa | Jumamosi |
|---|---|---|---|---|---|
| Tiro | Majembe | misumari | sukari | viberiti | mchele |
| Kanyau | Misumari | Misumari | viberiti | sukari | viberiti |
| Godi | sukari | viberiti | viberiti | sukari | mchele |
| Andanje | mchele | misumari | misumari | misumari | mchele |

18. Ni mteja gani wa Mzee Tamaa ambaye hununua bidhaa ambayo hainunuliwi na wateja wengine?

A. Tiro

B. Kanyau

C. Godi

D. Andanje

19. Tambua mteja wa Mzee Tamaa ambaye hununua bidhaa za aina mbili pekee,

A. Kanyau

B. Tiro

C. Andanje

D. Godi

20. Chagua jibu lenye siku ambayo kila mteja wa Mzee Tamaa hununua bidhaa inayotofautiana na ya wenzake.

A. Jumatano

B Jumanne

C. Alhamisi

D. Jumamosi



CamScanner

## SEHEMU B: SARUFI

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 21 hadi 25.**

(*Asubuhi. Obonyo yumo sebuleni mwao anaendelea kunadhifisha nyumba kwa sababu anatarajia wageni. Leo ni siku ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa.* Mlango unabishwa*)*.

**Obonyo** : (*Akielekea kufungua mlango*) __21__ .

**Memba** : (*Kwa furaha*) Leo nimekuletea zawadi ya kuadhimisha siku yako ya kuzaliwa.

**Obonyo** : (*Mshangao*) Kweli! Asante ndugu.Sikutarajia zawadi mapema hivi. Nimefurahia

**Memba** : Nilijua utafurahi sana. Ndio maana nikaichagua...

**Obonyo** : (*Anamchachawiza*) Wacha niifungue mwenyewe nijionee (*akifungua boksi*) Aha! Simu! Memba, umeninunulia simu? (*Machozi yanamtiririka*) Ndoto yangu imetimia. Nimekuwa nikitamani sana kuwa na simu ili niwe nikitumia kusakura utafiti tunaoambiwa tufanye na mwalimu wetu wa kiswahili. Mtandaoni. Nimekuwa nikifeli kufanya kwa sababu ya kukosa kifaa kama hiki. Umenifaa ndugu. Kweli __23__ .

**Memba** : (*Wakikumbatiana* ) Nimefurahi kuwa umeipenda

**Obonyo** : Nimeipenda kabisa. Ni kama ulisoma akili yangu ukajua rangi niipendayo. Rangi yenyewe ni ile ile yangu. Rangi ya zambarau. Rangi ya nakshi. Rangi ya kuvutia rangi yenye kufungua moyo.

**Memba** : Sikujua una kipawa cha ushairi. Umekariri shairi tamu sana. (*wote wanacheka*)

**Obonyo** : (*Anabofya nambari ya Teresia, mara Teresia anasikia ule upande mwingine*) Hallo

**Teresia** : (*Akicheka*) Hallo.

**Obonyo** : Je, hujambo? Kumbuka leo ni siku yangu kubwa sana. Siku ya kuadhimisha siku yangu ya kuzaliwa. Usikose kuja. Sherehe itaanza saa kumi alasiri.

**Teresia** : Una raha kweli! Nitahudhuria...!

**Obonyo** : (*Anakata simu ile*) Mwandani. Njoo,unisaidie kumaliza maandalizi. Mengi tutamaliza baadaye.

(***Wote wanaelekea jikoni***)

---

**21.** Chagua jibu sahihi kukamilisha nafasi ya 21 iliyoachwa kwenye kifungu...

A. Ingia

B. Kuja

C Karibu

D. Mlango u wazi

**22.** Kulingana na mazungumzo :

A. Wazungumzaji walifahamishana majina walipokutana...

B. Wanaozungumza walipanga kusherehekea sherehe zao pamoja

C. Obonyo na Memba wanaelekea kwao Teresia kumzawadi Simu

D. Mazungumzo yao yanaonyeshá kuwa wana uhusiano mwema

**23.** Chagua semi inayofaa kujaza nafasi ya 23 katika kifungu

A. Ndugu ni kufaana si kufanana

B. Mgaagaa na upishaani wali

C. Akiba haiozi

D. Mgala muwe na haki umpe



CamScanner

**24.** Unafikiri ni kwa nini Obonyo analia?

A. Kwa kuwa alinunuliwa simu ambayo hakutarajia

B. Imekuwa ni siku yake ya kwanza kutumia simu

C. Kwa sababu kitu ambacho amekuwa akitamani amekipata leo

D. Ni siku yake ya kuzaliwa

**25.** Memba alitambua kuwa Obonyo ni mtunzi na mwimbaji wa mashairi. Kwa hivyo Obonyo ni:

A. Sogora

B. Malenga

C. Manju

D. Mghani

**Kifungu kifuatacho kina nafasi 26 hadi 35. Umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kujaza nafasi.**

Kadri miaka ___26___ kusonga, ___27___ mabadiliko ___28___ kushuhudiwa kote ulimwenguni. Moja kati ___29___ ni ukuaji wa teknolojia. Teknolojia ni mojawapo ya njia ___30___ huonyesha kuwa ulimwengu ___31___ sio tu katika elimu ___32___ katika ___33___ mbalimbali za ___34___. Hata hivyo wengine hutumia maarifa hayo visivyo. Wahenga husema kuwa ___35___; yaani chochote kilicho na faida hakikosi hasara.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 26. | A. inazidi | B. inayozidi | C. inavyozidi | D. zinavyozidi |
| 27. | A. ndivyo | B. ndio | C. ndipo | D. ndiko |
| 28. | A. yanazidi | B. yanavyozidi | C. inavyozidi | D. zinavyozidi |
| 29. | A. hilo | B. yacho | C. yao | D. yayo |
| 30. | A. ambayo | B. ambao | C. ambalo | D. ambazo |
| 31. | A. umepiga konde | B. umetia shime | C. umepiga hatua | D. umepiga mbiu |
| 32. | A. mbali pia | B. bali pia | C. maadamu | D. hivyo basi |
| 33. | A. himaya | B. tabaka | C. dunia | D. nyanja |
| 34. | A. baraza | B. rai | C. aushi | D. ujira |

35. A. hakuna mchele ukosao ndume B. wapishi wengi huharibu mchuzi
C. Zito hufuatwa na jepesi D. Siku za mwizi ni arubaini

**Kutoka swali la 36 hadi la 50. Chagua jibu sahihi**

**36.** **Chagua wingi wa:**

Mtume na Karani wameondoka sokoni.

A. Watume na Karani wameondoka sokoni

B. Mitume na makarani wameondoka masokoni.

C. Mitume na makarani wameondoka sokoni

D. Watume na makarani wameondoka masokoni

**37.** Matunda, mimea na madawati ni nomino za kawaida.

Je, maneno chumvi, sukari na maziwa ni mfano wa nomino za:

A. dhahania B. makundi

C. wingi D. pekee

**38.** **Kanusha:**

Kabati lililoharibika limekarabatiwa.

A. Kabati lililoharibika halijakarabatiwa

B. Kabati lisiloharibika halikarabatiwi

C. Kabati lililoharibika halita karabatiwa

D. Kabati lisiloharibika halijakarabatiwa.



CamScanner

39. Rafiki yako amefiwa na wazazi wake licha ya maombi aliyokuwa akiwaombea kila siku. Utatumia methali gani kuonyesha kuwa alilopanga Mungu binadamu hawezi kulibadilisha?

A. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi
B. Usiache mbachao kwa msala upitao
C. Bidii ya mja haiondoi kudura.
D. Gangaganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini.

40. Chagua kiambishi sahihi kukamilisha nafasi katika sentensi ifuatayo:

**Nyasi ndefu _______ likatwa kwa fyekeo**

A. i B. zi
C. li D. vi

41. Maneno dhibiti na thibiti yana sauti zinazokaribiana. Je, ni neno lipi lenye sauti zinazokaribiana kimatamshi na neno ghani.

A. dhani B ghamu
C. gani. D. ramani

42. Chagua sentensi sahihi.

A. Mle ndimo mlipasafishwa.
B. Kule ndiko anakofanya kazi.
C. Kule ndiko anapofanya kazi
D. Pale ndiko anakofanya kazi

43. Chagua kitenzi kilicho katika kauli ya kutendesha.

A. Ponya B. Leweshwa
C. Cheza cheza D. Tembelea

44. Tambua kihisishi katika sentensi ifuatayo: Ala! Kumbe mjomba anaishi karibu na halati küle mjini?

A. Karibu na B. Kumbe
C. Mjini D. Ala!

45. **Chagua neno lifaalo kujaza pengo.**

Kalombotole atakuonyesha _______chakula hicho.

A. alipopika B. aliopika
C. alivyopika D. aliyopika.

46. Chagua neno sahihi kujaza nafasi katika jedwali lifuatalo.

| | |
|---|---|
| Usiku | mchana |
| Imara | _______ |

A. thabiti B. legevu
C. rahisi D. nyembamba

47. Ni sentensi gani inayoonyesha hali ya kuagiza?

A. Alikuwa akisoma gazeti nilipowasili.
B. Angesoma kwa bidii angefaulu.
C. Akifika mapema atampata ofisini.
D. Meza tembe tatu mara moja.

48. Ikiwa mtondogoo itakuwa Ijumaa, leo ni

A. Jumatatu B. Jumanne
C. Jumatano D. Jumamosi

49. **Tegua kitendawili:**

Hushindana wakifuatana.

A. Mawingu B. Miguu
C. Magurudumu D. Kivuli

50. Chagua usemi wa taarifa wa: **"Ukija mapema nitaweza kukutembeza humu mwetu,"** Pili alisema.

A. Pili alisema kuwa angekuja mapema angeweza kumtembeza humu mwao.
B. Pili alisema kuwa akija mapema ataweza kumtembeza humu mwao
C. Pili alisema kuwa angekuja mapema angeweza kumtembeza humo mwao
D. Pili alisema kuwa akija mapema ataweza kumtembeza humo mwao



CamScanner

# TARGETER WINGS

# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

# GREDI YA NANE - 2026

Wings 001

# KISWAHILI (Insha na Utangulizi wa Fasihi)

**MUDA: Saa 1 dakika 45**

| | |
|---|---|
| **Jina la Mwanafunzi** ____________________ | **Nambari ya Mwanafunzi** __________ |
| **Jina ya Shule yako** ____________________ | **Nambari ya Shule** __________ |
| **Sahihi ya Mwanafunzi** ____________________ | **Tarehe** __________ |

**KISWAHILI (Insha na Utangulizi wa Fasihi)**
**Karatasi ya 2**

**MAAGIZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako na nambari yako ya mtihani kwenye nafasi iliyoachwa hapo juu.
2. Andika jina na nambari ya shule yako kwenye nafasi iliyoachwa hapo juu.
3. Tia sahihi kwenye nafasi iliyoachwa hapo juu.
4. Andika tarehe ya mtihani ipasavyo.
5. Karatasi hii ina sehemu mbili; A na B.
6. Jibu maswali yote.
7. Andika majibu yote kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
8. Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| **SEHEMU** | **A** | **B** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **ZOEZI I** Swali:1 | **ZOEZI II** Swali 2: | **Zoezi III** Swali 3: | **Zoezi IV** Swali 4: | |
| **Alama ya upeo** | **15** | **15** | **10** | **10** | |
| **Alama ya Mwanafunzi** | | | | | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**
**Wanafunzi ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**SEHEMU A (Alama 15)**

**ZOEZI I : INSHA**

**Maagizo**

(i) Inapendekezwa uchukue muda wa dakika 40 katika zoezi hili.

(ii) Andika insha yenye maneno kati ya 300 - 350 katika nafasi uliyoachiwa.

**Andika insha ya kusisimua kuhusu sherehe ya kufana uliyohudhuria.**



CamScanner

## **SEHEMU B** (Alama 35)

**ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)**

**2. Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Wakulima ongezeni kilimo x 2
Twahitaji wananchi wawe na afya
Wakulima ongezeni kilimo
Wafugaji pia ongezeni mifugo
Wananchi wote muwe na afya njema

Kuleni mayai, maziwa na maharagwe
Pia na mbaazi, nyama samaki
Hivi ni vyakula bora vya kujenga mwili.

a) Eleza sababu **mbili** za kuimba wimbo wa aina hii. **(alama 2)**

b) Wimbo huu una ujumbe gani? **(alama 2)**

c) Eleza mitindo **mitatu** ya kuwasilisha wimbo huu. **(Alama 3)**

d) Vyakula vilivyotajwa vina umuhimu gani kwa binadamu? **(alama 2)**

e) Bainisha kipera cha wimbo huu. **(alama1)**

**3.** a) Eleza umuhimu wa ploti katika kazi ya fasihi. **(alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

b) Eleza sifa **mbili** za fasihi simulizi. **(alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

c) Fafanua maana ya **fanani.** **(alama 1)**

______________________________________________

## ZOEZI III : NOVELA

**3. Soma sehemu ifuatayo ya novela kisha ujibu maswali**

Walifika mjini na kufululiza moja kwa moja hadi kwenye jumba moja lililokuwa limeandikwa 'Tumaing' mall. Huko kulikuwa kunauzwa bidhaa za kila aina. Shangazi aliwaambia Herina na mama yake watangulie au watembee ubavuni mwake. Hakutaka wawe nyuma yake. Herina alielewa kiina cha agizo hilo. Adabu yake haikumruhusu kuuliza. Alijua kwamba ipo siku ambapo yeye na shangazi yake wangeambiana ukweli.

Walitembea kimya kimya kwa muda, Herina akiwa mbele, hadi shangazi alipomwita kwa sauti na kumwambia asimame. Walikuwa wamefika kwenye duka moja, ambalo liliuza nguo. Mlangoni palikuwa na maneno **"Designer wear"**. Shangazi aliwaashiria waingie humo dukani. Alisalimiana na muuzaji kwa furaha na bashasha. Herina alipowaangalia aling'amua kwamba walifahamiana. Muuzaji aliwaashiria Herina na mama yake waketi kwenye viti vya kisasa vilivyokuwa karibu na mahali pa kujipimia nguo. Shangazi alisema. "Ndiye huyu. Uonavyo si mdogo wala mkubwa sana. Natumai tutapata nguo zinazomtoshea.

a) Tambua aina **mbili** za mandhari zinazojitokeza katika sehemu hii ya novela. **(Alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

b) Eleza sifa **mbili** za Herina kulingana na sehemu hii ya novela. **(Alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

c) Eleza ploti ya sehemu hii ya novela. Ukizingatia kuwa ploti ni mfuatano wa matukio katika kazi ya fasihi (Alama 2)

d) Eleza mbinu **mbili** za lugha zilizotumiwa katika Sehemu hii ya fasihi. (Alama 2)

e) Taja Masuala **mawili** ambayo yameshughulikiwa katika sehemu hii ya novela. (Alama2)

**ZOEZI IV: USHAIRI (Alama 10)**

**4. Soma shairi ifuatayo ya tamthilia kisha ujibu maswali.**

Tazama yaliyo mbele, nyuma itakumaliza,
Yaliyopita si ndwele, yasikuletee giza,
Yasikuletee giza, tazama yaliyo mbele.

Tazama yaliyo mbele, na hayo kufwatiliza,
Achana na zile ole, majuto yanaumiza,
Majuto yanaumiza, tazama yaliyo mbele.

Tazama yaliyo mbele, unaweza kugeuza,
Usirudi nyuma kule, nyuma kulishakuliza,
Nyuma kulishakuliza, tazama yaliyo mbele.

Tazama yaliyo mbele, nguvu zote kuingiza
Mbele ina tunu tele, mbele ina miujiza
Mbele ina miujiza, tazama yaliyo mbele.

a) Eleza ujumbe unaotolewa na shairi hili. (Alama 2)

________________________________________

________________________________________

b) Shairi hili ni la aina gani? Toa Sababu (Alama 2)

________________________________________

________________________________________

c) Bainisha mbinu **mbili** za lugha zinazojitokeza katika shairi hili. (Alama 2)

________________________________________

________________________________________

d) Taja migao **miwili** ya shairi hili. (Alama 2)

________________________________________

________________________________________

e) Tambua masuala **mawili** ambayo yameshughulikiwa katika shairi hili. (Alama 2)

________________________________________

________________________________________



CamScanner